(81)

WIZARA YA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO
TAASISI YA SANAA NA UTAMADUNI BAGAMOYO
(TaSUBa)

RECEIVED
DATE 28/.03/2018

Simu: +255 232 440 032,
Barua pepe: tasuba@habari.go.tz
Tovuti: www.tasuba.ac.tz
Unapojibu tafadhali taja:

S.L.P. 32,
Bagamoyo

27 Februari, 2018.

Kumb. Na. HUSM/TSUB/MF.5/40.

Mkurugenzi Mtendaji,
Halmashauri ya Wilaya/~~Mji~~/~~Manispaa~~/~~Jiji~~ ....NSIMBO....,
S.L.P.........................,
.......NSIMBO....... - **Aione Afisa Utamaduni**

DAHRO

**YAH: TANGAZO LA KUJIUNGA NA CHUO**

Rejea kichwa cha habari tajwa hapo juu.

Taasisi ya Sanaa na Utamaduni Bagamoyo (TaSUBa) inakuomba wewe na ofisi yako kutusaidia kusambaza tangazo la nafasi za kujiunga na chuo ambazo zitaanza kufundishwa mwaka wa masomo 2017/2018 kwa Muhula wa Aprili 2018.

Kwa kutambua umuhimu wako katika sekta ya Sanaa na Utamaduni, Taasisi vilevile inakuomba kwa heshima na taadhima kutusaidia kutangaza nafasi hizo katika ngazi za chini kama vile Tarafa, Kata, na kwingineko kwa kutoa nakala na kubandika katika mbao za matangazo na sehemu nyingine husika.

Tangazo husika limeambatanishwa pamoja na barua hii.

Natanguliza shukrani zangu za dhati kwako na ni matumaini yangu kuwa ombi letu litafanyiwa kazi.

Wako katika kuendeleza Sanaa na Utamaduni,

Izengo Joseph
kny: MTENDAJI MKUU